

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 16 Juni, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu Taarifa ya Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 91(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 30(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kuwajulisha kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, leo hii atalihutubia Bunge katika kuhitimisha uhai wa Bunge hili la Kumi na Moja ambalo shughuli zake zitafungwa leo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo tutaruhusu ili wageni wetu waweze kuingia. Kwa sababu hiyo, na mimi hapa nitaahirisha Bunge baada ya muda mfupi ili tuweze kutoa fursa hiyo na Mheshimiwa Rais pia kuingia humu ndani.

Baada ya kusema hayo niwaombe wote mtulie, msitoke humu ndani nitakapositisha shughuli za Bunge kwa muda mfupi, kwa hiyo kila mtu abaki sehemu yake tusiendelee kuzunguka kwa sababu viongozi wanaanza kuingia sasa.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka muda mfupi ujao.

(Saa 3.02 Asubuhi Bunge lilitishwa kwa muda mfupi)

NDG. PATSON SOBHA - OFISA WA BUNGE:
Waheshimiwa Wabunge, msafara ambaa unatanguliwa na Mpambe wa Bunge lakini unaongozwa na Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga unaelekeea ndani. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga anafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkoo wa Tanzania, akifuatiwa na Mheshimiwa Omar Othman Makungu, Jaji Mkoo wa Zanzibar na Makatibu Mezani Ndugu Joshua Chamwela na Ndugu Asia Ninja. (Makofi/Vigelegele)

*(Hapa Msafara wa Jaji Mkoo wa Tanzania - Jaji Profesa Ibrahim Hamis Juma na Jaji Mkoo wa Zanzibar - Jaji Omar Othman Makungu ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bunge
Mhe. Najma Murtaza Giga Uliingia Ukumbini)*

*(Hapa Msafara wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar -
Mhe. Balozi Seif Ali Idd na Spika wa Baraza la Wawakilishi -
Mhe. Zuberi Ali Maulid ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bunge
Mhe. Andrew John Chenge Uliingia Ukumbini)*

*(Hapa Msafara wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya
Muungano wa Tanzania - Mhe. Samia Suluhu Hassan na
Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Ali
Mohamed Shein ukiongozwa na Naibu Spika wa Bunge -
Mhe. Dkt. Tulia Ackson Uliingia Ukumbini)*

NDG. PATSON SOBHA - OFISA WA BUNGE:
Waheshimiwa Wabunge, viongozi wakuu wa kitaifa, wageni

waalikwa, mabibi na mabwana naomba tuketi tukisubiri utaratibu unaoendelea.

Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge, leo kwa kweli ni neema ya peke yake, tuna viongozi wakuu wasataafu ambao baadae Mheshimiwa Spika atatangaza uwepo wao lakini pia Mabalozi na wageni waalikwa mbalimbali. *Gallery* zetu leo hazitosh kabisa, kwa hiyo, naomba nitangaze kwamba wale ambao wamekosa nafasi kwenye *gallery* Ukumbi wa Pius Msekwa mtaendelea kuona Bunge na mtashuhudia kila kitu. Kwa hiyo karibuni sana na muelekee Ukumbi wa Pius Msekwa, kuna Maafisa Itifaki wa Bunge watawaongoza kuelekea kule wale ambao mmekosa kabisa nafasi za kuketi katika *gallery* za ukumbi huu.

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana, Mheshimiwa Rais tumeshuhudia ameshawasili, anapokea gwaride la heshima, atakagua na kisha ataaelekea Chumba cha Mavazi cha Spika (*Robing Room*) na baada ya muda si mrefu ndipo ataingia ndani ya ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kazi moja tu kubwa ya kuhitimisha maisha ya miaka mitano ya Bunge la Kumi na Moja na panapo majaliwa mwezi Novemba, 2020 Mungu akitoa nafasi litakuja Bunge la Kumi na Mbili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Rais ameshapokea gwaride la heshima na amekagua na sasa anasalimiana na viongozi ambalo walikwenda mpokea, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyevit wa Bunge, Katibu wa Bunge na Wakuu wa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Rais anaaelekea moja kwa moja kwenye chumba cha kuvalia mavazi Mheshimiwa Spika kwa dakika chache na kisha wataingia ndani ya ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge atamuongoza Mheshimiwa Rais kuingia ndani ya Bunge na huo utakuwa msafara wakiwa wametanguliwa na Mpambe wa Bunge na atakuwepo pia Naibu Spika katika msafara huo na Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na

Ndugu Nenelwa Mwihambi - Katibu Mezani, hizo zitakuwa ni dakika chache baada ya hapo.

Wakishaingia ndani ya ukumbi wa Bunge, utaratibu utakuwa kama ifuatavyo na nilishasema awali kwamba Dua itasomwa, kisha Taarifa ya Spika itasomwa na kisha atamkaribisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aweze kulihutubia Bunge.

Mheshimiwa Rais atalihutubia Bunge na kulifunga na baada ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Spika atatoa maneno ya shukurani kwa Mheshimiwa Rais pamoja na kutambulisha wageni walipo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitapigwa hizi nyimbo mbili na kuimbwa. (*Makofii*)

Baada ya Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki kuimbwa, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji hadi siku litakapoitishwa tena kwa mujibu wa Katiba.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kutoka ukumbini utakuwa kama ifuatavyo; msafara wa kwanza utatoka ukumbini ukitanguliwa na Mpambe wa Bunge, ukiongozwa Mheshimiwa Spika na kaisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katibu wa Bunge na Katibu Mezani wataelekea kwenye lango kuu kwa ajili ya kuagana.

Baada ya Mheshimiwa Rais kuondoka, Mheshimiwa Spika atabaki kuagana na viongozi wengine ambao sasa wapo ukumbini.

Msafara wa pili utatoka ukumbini ukitanguliwa na Mpambe wa Bunge na kuiongozwa na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, akifuatiwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kisha Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein - Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na watafuatiwa na Makatibu Mezani.

Msafara wa tatu utatoka ukumbini ukitanguliwa na Mpambe wa Bunge na kuongozwa na Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Andrew John Chenge, akifuatiwa na Balozi Seif Ali Idd - Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kisha Makatibu Mezani.

Msafara wa nne utatoka ukumbini ukitanguliwa na Mpambe wa Bunge na kuongozwa na Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga akifuatiwa na Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mheshimiwa Mustafa Mohamed Siami - Jaji Mfawidhi wa Dodoma na Makatibu Mezani. (*Makof*)

Baada ya misafara yote ya viongozi, Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoka nje ya Ukumbi wa Bunge na kufuatiwa na Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao watatoka kwa utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge shughuli yangu kwa kweli inakomea hapa na panapo majaliwa inawezekana katika Bunge la Kumi na Mbili niktapewa kazi hii tena. Nitashukuru Mungu maana mimi nipo hapa hapa. (*Makof*)

(Bunge Lilirudia Saa Nne Asubuhi)

(Hapa Msafara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli ukiongozwa na Spika wa Bunge Mhe. Job Yustino Ndugai, Ulliingia Ukumbini)

WABUNGE FULANI: CCM! CCM! CCM! (*Makof/ Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: Chuma! Chuma! Chuma! (*Makof/ Vigelegele*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae sasa.

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wageni wetu wote waalikwa, naomba nianze na kutoa Taarifa ya Spika kwamba katika Mkutano tuliomaliza jana, Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, Bunge lilikuwa limepitisha miswada sita ya sheria ya Serikali katika Mkutano huo wa Kumi na Tisa tuliomaliza jana.

Muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2020 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2) Bill, 2020*],

Wa pili ni Muswada wa Sheria ya Afya ya mimea wa mwaka 2020 (*The Plant Health Bill, 2020*),

Wa tatu ni Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa Mwaka 2020 (*The Deep Sea Fisheries Management and Development Bill, 2020*), (*Makofi*)

Wa nne ulikuwa ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2020 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2020*]. (*Makofi*)

Wa tano ni Muswada wa Matumizi ya Fedha za Serikali wa mwaka 2020 (*The Appropriation Bill, 2020*) (*Makofi*)

Na muswada wa mwisho, wa sita kwa Bunge liliopita hili ni Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2020 (*The Finance Bill, 2020*). (*Makofi*)

Kwa utendaji kazi wa Mheshimiwa Rais wa namna isiyokuwa na ulinganifu, tayari amekwishatia sahihi miswada yote hiyo sita ikiwa ni pamoja na ile sheria ambayo tumemaliza jana usiku kwenye saa mbili, Sheria ya Fedha, Sheria Na. 8 ya mwaka 2020 (*The Finance Act No. 8, 2020*) na yenye we imeshatiwa sahihi tayari. (*Makofi/Vigelegele*)

Kwa hiyo, kwa ajili ya kumbukumbu zetu kwenye *Hansard*, naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba miswada yote hiyo imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo ni sheria za nchi zifuatazo:-

Kwanza ni Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2, Sheria Na. 3 ya mwaka 2020 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2), Act No. 3 of 2020*];

Sheria ya Afya ya Mimea, Sheria Na. 4 ya mwaka 2020 (*The Plant Health Act No. 4 of 2020*);

Ya tatu ni Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuu wa Bahari Kuu, Sheria Na. 5 ya mwaka 2020 (*The Deep Sea Fisheries Management and Development Act No. 5 of 2020*); (*Makofii*)

Ya nne Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3, Sheria Na. 6 ya mwaka 2020 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Act, Act No. 6 2020*];

Ya tano ni Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, Sheria Na. 7 ya mwaka 2020 (*The Appropriation Act No. 7 of 2020*); na

Ya sita ni Sheria ya Fedha, Sheria Na. 8 ya mwaka 2020 (*The Finance Act, Act No. 8 2020*). Hilo ni jambo la kwanza nilitaka tufunge kabisa shughuli za Mkutano wa Kumi na Tisa, kwamba hakuna kiporo. (*Makofii*)

Sasa Mheshimiwa Rais toka ulivyokuja tarehe 20 Novemba, 2015 kulifungua Bunge hili na kulipa idhini ya kuanza shughuli zake Kikatiba, kwa kweli kazi nydingi sana zimefanyika kwenye Bunge hili, nitaje tu baadhi; Miswada iliyopitishwa na Bunge hili la Kumi na Moja yote kwa ujumla wake ni miswada 60 na yote imepata kibali cha Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, sheria hizi 60 ni sheria halali za nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Rais, Maazimio yaliyopitishwa na Bunge jumla yake ni 38. (*Makofii*)

Mheshimiwa Rais, maswali ya msingi yaliyoulizwa Serikalini na Waheshimiwa Wabunge na kupata majibu kutoka Serikalini ni 3,376 na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu 172. (*Makofii*)

Mheshimiwa Rais, tuliunda Kamati Maalum za ushauri kwa Serikali nne ambazo ni Kamati ya Masuala ya Tanzanite, Kamati ya Masuala ya Almasi, Kamati ya Masuala ya Gesi Asilia na Kamati ya Masuala ya Uvuvi wa Bahari Kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Rais, tumeifanya kazi, tumeitenda kazi, Wabunge hawa wameatumikia Watanzania kwa uaminifu mkubwa sana. Wamenipa ushirikiano mkubwa sana, na mimi kwa niaba yao najua kuna wakati Bunge hili huwa linachemka kama bahari, lazima kuna wakati tulikuudhiudhi kidogo Mheshimiwa Rais, basi ni katika mchakato huu wa mambo yenye we ya Kibunge yalivyo maana ukumbi huu ni ukumbi wa minyukano kidogo na kadhalika, lakini mwisho wa siku yote ni mema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Rais, kwa heshima na taadhima sasa naomba nikukaribishe ili uweze kulihutubia Bunge hili na kupitia kulihutubia Bunge hili, ulihutubie Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Rais, karibu sana. (*Makofii*)

HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyetujalia uhai na kutuwezesha kuionna siku ya leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu wapo wenzenetu ambao tulikuwa nao wakati wa kuzindua Bunge hili

lakini leo hatuko nao, wametangulia mbele ya haki. Hivyo basi, kwa heshima yao naomba tusimame kwa dakika moja kuwakumbuka.

(Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja kuwakumbuka waliotangulia mbele ya haki)

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mwenyezi Mungu azipumzise roho zao mahali pema peponi, Amina. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea zaidi, naomba kutambua uwepo wa viongozi mbalimbali kwenye ukumbi huu na nimefurahi kuwaona Waheshimiwa Marais wetu Wastaafu wote wapo hapa pamoja na Makamu wa Rais Mstaafu na pia Mawaziri Wakuu Wastaafu akiwemo Mheshimiwa Edward Lowassa na Mheshimiwa Frederick Sumaye; hii ndiyo Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefurahi pia kuwaona viongozi wa dini, majaji na viongozi mbalimbali na tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda nikushukuru wewe, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa kunipa kibali cha kuja kulihutubia Bunge hili. Aidha, nawashukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga kwa ushirikiano wenu; ahsanteni sana. Hiki ni kielelezo cha uhusiano mzuri uliokuwepo katika mihimili yetu mitatu katika kipindi chote cha miaka mitano iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kueleza kuwa tangu nimeingia ndani ya Bunge hili leo nimeshuhudia mabadiliko mengi makubwa sana, tofauti na ilivyokuwa wakati mimi nikiwa Mbunge. Hivi sasa nimeona hata Waheshimiwa Wabunge wanatumia vifaa vya kisasa kama vile *tablets*, enzi zetu vifaa hivyo havikuwepo. Hivyo basi,

nakupongeza sana kwa ubunifu huu na ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuweza kuvitumia vifaa hivi na hivyo kulifanya Bunge letu kuwa la kisasa na la namna ya pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Novemba, 2015 nilikuja kuzindua Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo tena kwa madhumuni ya kutimiza matakwa ya Katiba yetu nimekuja kulihutubia kwa mara ya mwisho ili hatimaye kuweza kuruhusu kuanza kwa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa wakati nikizindua Bunge lako tukufu nilitumia fursa hiyo pia kutoa mwelekeo, kueleza malengo na pia kutaja vipaumbele vyta Serikali ya Awamu ya Tano. Siku ile nakumbuka nilieleza mambo mengi sana ambayo nafarijika kuona kuwa mengi tumefanikiwa kuyatekeleza. Tumefanikiwa kuyatekeleza kama ambavyo Waheshimiwa Mawaziri mbalimbali walivoyeleza wakati wakiwasilisha bajeti zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye naye wakati wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali alitoa ufanuzi wa mafanikio tuliyoyapata. Aidha, jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelezo ya kina kuhusu mafanikio yaliyopatikana. Ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naweza kusema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumeweza kutimiza wajibu wetu kwa kuwatumikia Watanzania kwa kiasi kikubwa na tumeweza kufanya hivyo kutohana na ushirikiano mkubwa tuliuopata kutoka kwa Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa kuishauri vyema na pia kuisimamia vizuri Serikali katika kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Aidha, napenda pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Madiwani kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye maeneo yao. Kama mnavyofahamu Madiwani ni kiungo muhimu kati ya wananchi na Serikali, lakini pia kati yenu Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi mnaowaongoza, nawashukuru sana. Na kwa kutambua hivyo, hatuna budi kuwashukuru Waheshimiwa Madiwani wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie fursa hii kuwashukuru watangulizi wangu kuanzia Awamu ya Kwanza iliyooongozwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; Awamu ya Pili iliyooongozwa na Mzee Ali Hassan Mwinyi; Awamu ya Tatu iliyooongozwa na Mzee Benjamin William Mkapa pamoja na Awamu ya Nne iliyooongozwa na Mzee Jakaya Mrisho Kikwete. (*makofi*)

Mheshimiwa Spika, watangulizi wangu hawa waliweka misingi imara na kutengeneza mazingira yanayowezesha kupatikana mafankio hayo mbalimbali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu na katika hilo nawashukuru pia hawa viongozi wetu wakuu, Mzee wetu Mwinyi ambaye alijulikana kwa jina Mzee Ruksa, Mzee Mkapa alijulikana kwa jina la Mzee Ukweli na Uwazi na Mzee Kikwete alijulikana kama Mzee wa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Ninawashukuru kwa ushauri wao mbalimbali waliotupatia katika kipindi chote cha miaka mitano iliyopita. Nikiri tu kwamba ushauri wao umenisaidia sana mimi binafsi pamoja na Serikali ninayoongoza. Nawashukuru pia Makamu wa Rais Mstaifu, Marais wa Zanzibar Wastaifu na Mawaziri Wakuu Wastaifu kwa ushirikiano wao, ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama utakavyokumbuka, mojawapo ya ahadi kubwa niliyoitoa wakati wa kuzindua Bunge ilikuwa kudumisha amani, umoja, mshikamano, Mapinduzi matukufu ya Zanzibar pamoja na Muungano wetu na hali kadhalika kuimarisha amani, ulinzi, usalama na utulivu

wa nchi yetu. Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba tumeitimiza ahadi hiyo kwa vitendo. (*Makof*)

Watanzania tumeendelea kubaki kuwa wamoja na tumeendelea kushirikiana licha ya tofauti zetu za dini, kabilia, rangi, ufuasi wa vyama vya siasa au mahali tunapotoka. Muungano wetu pia umendelea kuimarika, tumeweza kushughulikia baadhi ya changamoto za Muungano na kufikia mafanikio na makubaliano ikiwemo kuhusu suala la gharama za kushusha mizigo (*landing fees*) na pia kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na malimbikizo ya kodi hiyo ya shilingi bilioni 22.9 ambayo Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) lilikuwa likidaiwa na TANESCO. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia tumefanikiwa kulinda mapinduzi matukufu ya Zanzibar. (*Makof*)

Kuhusu amani, ulinzi na usalama nchi yetu imeendelea kuwa kisiwa cha amani na mipaka yake imebaki kuwa salama. Utakumbuka kuwa wakati tukiingia madarakani kulikuwepo na wimbi kubwa la uhalifu wa kutumia silaha pamoja na vitendo vingine vya kihalifu ikiwemo matukio ya mauaji kule Kibiti na Rufiji. Hata hivyo, kutohana na kazi kubwa iliyofanya na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vitendo vyote hivyo vilikomeshwa na ninapenda niseme kwamba nchi yetu kwa sasa ipo salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha hilo Ripoti ya *Global Peace Index* ya mwaka 2020 imeitaja Tanzania kushika nafasi ya kwanza kwa amani na utulivu kwenye eneo la Afrika Mashariki na ya saba kwa nchi za Afrika zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara. (*Makof*)

Kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge na kwa niaba ya Watanzania wote navipongeza sana vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kusimamia amani nchini. Na ninawashukuru pia Watanzania kwa kutoa ushirikiano kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, ahsanteni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumejitahidi pia kuimarisha maadili, nidhamu na utendaji kazi Serikalini. Kama tulivyoahidi, hatutakuwa na mzaha kwa viongozi na watumishi wazembe walioshindwa kufanya kazi kwa weledi, nidhamu, maarifa na uadilifu. Viongozi na watumishi wa namna hiyo walichukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kuwatumbua, kuwashusha vyeo na mishahara au kuwapa onyo kali. (*Makof*)

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo jumla ya watumishi 32,555 wamechukuliwa hatua mbalimbali, wakiwemo watumishi 15,508 ambao waliachishwa kazi kwa kukutwa na vyeti nya kughushi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, tulifuta ajira hewa 19,708 zilizokuwa zinaigharimu Serikali kila mwezi kiasi cha shilingi billioni 19.8 hatua hili illitoa fursa ya kuajiri watumishi wapya wenye sifa wapatao 74,173. (*Makof*)

Vilevile kufuatia hatua tulizochukua tuliwapandisha vyeo watumishi 306,617 na kulipa madeni ya watumishi ya mishahara na yasiyo ya mishahara yenye thamani ya shilingi bilioni 472.6; ya kimshahara ni shilingi bilioni 114.5 na yasiyo ya kimshahara ni shilingi bilioni 358.1. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tulifanya haya kwa lengo la kulinda heshima ya wafanyakazi na kuleta nidhamu kwenye utumishi wa umma. Sambamba na kuimarisha nidhamu Serikali tulizidisha mapambano dhidi ya rushwa, uhujumu uchumi na ujisadi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa wakati nikizindua Bunge hili niliahidi kuanzisha Mahakama ya Uhujumu Uchumi, Mahakama hiyo ilianzishwa mwaka 2016 na mpaka sasa imepokea mashauri 407 ambapo mashauri 385 tayari yamesikilizwa na zaidi ya hapo katika kupambana na adui rushwa Taasisi yetu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeweza kufungua mashauri 2,256 ambapo mashauri 1,926 tayari yametolewa uamuzi na Serikali imepata ushindi kwenye mashauri 1,013. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita pia TAKUKURU imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 273.38 zikiwemo fedha walizokuwa wamedhulumiwa wakulima. Aidha, TAKUKURU imetaifisha fedha taslimu Shilingi milioni 899, Dola za Marekani 1,191,651; Euro 4,301,399; nyumba nane zenye thamani ya Shilingi bilioni 11.6, magari matano yenye thamani ya Shilingi milioni 126 pamoja na viwanja vitano. Aidha, tumeweza kurejesha mali za Serikali zilizochukuliwa na watu binafsi ama taasisi kinyume cha sheria zikiwemo nyumba na majengo 98 ikiwemo *Mbeya Hotel*, Mashamba 23, viwanja 298, kampuni tatu, maghala 69, vilevile kiasi cha fedha na mali zilizowekwa zuio zikisubiria kukamilika kwa taratibu za kisheria za utaifishaji ni Shilingi bilioni 52.7; Dola za Marekani milioni 55.8, Euro milioni 4.3, magari 75, nyumba 41, viwanja 47 na mashamba 13. Ninawashukuru sana TAKUKURU kwa kazi nzuri waliyoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii bila shaka inaonesha dhamira yetu isyo na mashaka ya kupambana na rushwa na ufisadi. Napongeza mhimili wa Mahakama, TAKUKURU, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, Jeshi la Polisi pamoja na wananchi kwa ujumla kwa kufanikisha mapambano haya. Lakini pia nitumie fursa hii pia, kuipongeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa kufanikisha kidhibiti na kuvunja mitandao ya biashara hiyo haramu. (*Makof*)

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita jumla ya tani 97.99 za bangi, tani 85.84 za mirungi, kilo 567.96 za *heroin* na kilo 23.383 za *cocaine* zimekamatwa pamoja na watuhumiwa 37,104. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ndizo zililifanya Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevyta na Uhali (UNODC) mwaka jana kuipongeza nchi yetu ya Tanzania kwa kupunguza uingizaji wa dawa za kulevyta kwa asilimia 90, lakini niseme Waheshimiwa Wabunge mafanikio haya yasingepatikana kama pasingekuwa na sheria nzuri zilizopitishwa na Bunge hili. Hivyo, basi kwa heshima kubwa nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyoifanya. Nawashukuru pia Watanzania kwa

ushirikiano waliota katika kukabiliana na biashara hii haramu ya dawa za kulevya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati nikizindua Bunge hili nilieleza kwa kirefu sana kuhusu kutoridhishwa kwangu na hali ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hivyo basi, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumejitahidi kushughulikia suala hilo kwa kusimamia uadilifu kwa watumishi waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kuimarisha sheria za kodi, mifumo, TEHAMA na kupanua wigo wa walipa kodi, kupunguza misamaha na kuziba mianya ya ukwepajji kodi na kadhalika. Kutohana na hatua hizo ukusanyaji wa mapato umeimarika, mathalani ukusanyaji wa mapato ya kodi kwa mwezi umeongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 mwaka 2015 hadi shilingi trilioni 1.3 hivi sasa. Na katika mwezi Disemba, 2019 *TRA* ilikusanya shilingi trilioni 1.987 kiwango ambacho ni cha juu kabisa kuwahi kukusanya kwenye historia ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande a mapato yasiyo na kodi nayo yameongezeka kutoka chini ya shilingi bilioni 688.7 mwaka 2014/2015 hadi kufikia shilingi trilioni 2.4 mwaka 2018/2019. Halikadhalika mapato ya ndani ya Halmashauri zetu nayo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 402.66 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 661 mwaka wa fedha wa 2019. Hii imefanya mapato ya ndani kwa ujumla yaongezeke kutoka shilingi trilioni 11.0 mwaka 2014/215 hadi shilingi trilioni 18.5 mwaka wa fedha wa 2018/2019. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato tumedhibiti matumizi ya fedha za Serikali kwa kuzuia au kupunguza safari za nje zisizo za lazima, semina, warsha, makongamano, matamasha na udanganyifu kwenye manunuzi. Aidha, tulipitia upya muundo wa Serikali ili kuongeza ufanisi na kubana matumizi yasiyo ya lazima. Katika zoezi hilo tuliweza kupunguza idadi ya Wizara kutoka 29 hadi 22 na pia tuliunganisha taasisi, idara na vitengo mbalimbali. Vilevile tumepitia miundo ya Wizara, taasisi na idara zinazojitegemea 116 na kufanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 17.4. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeunganisha pia mifuko ya hifadhi ya jamii kutoka mitano kuwa hifadhi za jamii miwili kwa lengo hilohilo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji. Mabadiliko haya yalifanyika baada ya kupata baraka za Bunge hili tukufu, hivyo nina haki kabisa ya kusema ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, bila ninyi haya yote yasingefanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya kuongezeka kwa mapato na kudhibiti matumizi, Serikali iliweza kuongeza bajeti ya maendeleo kutoka wastani wa asilimia 26 hadi asilimia 40. Hii ndio imetuwezesha kuboresha huduma mbalimbali za jamii na kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo; kwa upande wa huduma za jamii tumepanua wigo na kuboresha upatikanaji wa huduma za elimu, afya pamoja na maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye elimu kama unavyofahamu tulianza kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari ambapo mpaka mwezi Februari, 2020 tulikuwa tumetumia shilingi trillioni 1.01 kugharamia, lakini mbali na kutoa elimu bure tumeongeza idadi ya shule za msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka huu. Shule za sekondari nazo zimeongezeka kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi shule 5,330 mwaka wa 2020.

Vilevile tumekarabati shule kongwe za sekondari, tumekarabati shule 73 kati ya shule 89, tumejenga mabweni 253 na maabara 227. Aidha, tumetoa vifaa vya maabara vipatavyo 2,956 na tumeponguzza kiasi kikubwa cha tatizo la uhaba wa madawati ambapo idadi yake imeongezeka kutoka madawati 3,024,311 mwaka 2015 hadi kufikia madawati 8,095,207. Ongezeko hili ni sawa na kuongezeka kwa asilimia 200. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vyuo vya ualimu, tumekarabati vyuo 18, tumejenga upya vyuo viwili vya Murutunguru na Kabanga na hali kadhalika tumepeleka *computer* 1,550 kwenye vyuo vyote 35 vya ualimu. Lengo ni kuimarisha ufundishaji wa masomo ya TEHAMA. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ngazi nyingine za elimu; tumeongeza Vyuo vya Ufundı (*VETA*) kutoka 672 mwaka 2015 hadi 712 mwaka 2020. Na pia tumekarabati na kuboresha vifaa na miundombinu ya kufundishia katika vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (*FDC*).

Mheshimiwa Spika, vilevile tumejenga hosteli, kumbi za mihadhara, mabwalo ya chakula na maktaba kwenye vyuo vikuu. Tumeongeza pia bajeti ya mikopo ya elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 348.7 mwaka 2014/2015 hadi shilingi bilioni 450 mwaka huu wa fedha wa 2019/2020. Kutokana na hatua hizo uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza umeongezeka maradufu kutoka wastani wa wanafunzi milioni 1 mwaka 2015 hadi kufikia milioni 1.6 hivi sasa. (*Makofı*)

Mheshimiwa Spika, aidha, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne imeongezeka kutoka 1,648,359 mwaka 2015 hadi 2,185,037. Idadi ya wanafunzi wa *VETA* nayo imeongezeka kutoka 117,067 mwaka 2015 hadi 226,767 mwaka wa 2020 na idadi ya wanafunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDC*) imeongezeka kutoka 6,693 mwaka 2016/17 hadi 9,736 mwaka 2018. (*Makofı*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vyuo vikuu idadi ya wanafunzi wanaojiunga mwaka wa kwanza imeongezeka kutoka 65,064 mwaka 2015 hadi 87,813 mwaka 2020 na wenye kupata mikopo nao wameongezeka kutoka 98,300 mwaka 2014/2015 hadi 130,883 mwaka 2019/2020. Kwa taarifa hii Waheshimiwa Wabunge naamini itakuwa sijakosea nikisema kazi kubwa imefanyika kwenye sekta ya elimu. (*Makofı*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya afya, tumeongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya 1,769 zikiwemo zahanati 1,198 vituo vya afya 487 ambavyo ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi katika majimbo yenu. Hospitali za Wilaya 71, Hospitali za Mikoa 10 ikiwemo Hospitali ya Mkoa wa Mara ambayo ni *Mwalimu Nyerere Memorial Hospital* ambayo ujenzi wake ulikwama tangu miaka ya 1970. (*Makofı*)

Waheshimiwa Wabunge, vilevile tumejenga Hospitali za Rufaa za kanda tatu. Hii imefanya vituo vyatolea huduma za afya kuongezeka kutoka 7,014 mwaka 2015 hadi kufikia 8,783 hivi sasa. Zaidi ya hapo, tumeajiri watumishi wa afya wapya wapataao 14,479 wakiwemo madaktari 1,000 walioajiriwa hivi karibuni. Hii imeongeza idadi ya watumishi wa afya nchini kutoka 86,152 mwaka 2015 hadi 100,631 mwaka 2020. Tumeimarisha pia upatikanaji wa dawa, vifaa tiba ambapo tuliongeza bajeti yake kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 270 hivi sasa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, pia tumenunua na kusambaza magari ya kubebaa wagonjwa (*ambulance*) 117. Vilevile tumefanikiwa kusomesha madaktari bingwa 301 ambaa wamewezesha kuimarisha matibabu ya kibingwa nchini hususan kwa magonjwa ya moyo, masikio, figo, mifupa, ubogo, kansa na kadhalika. Kutokana na hatua hizo, idadi ya akina mama wanaojifungua kwenye vituo vyatolea huduma za afya imeongezeka kutoka asilimia 60 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 83 hivi sasa. Vifo vyatolea wachanga wenye chini ya siku 28 vimepungua sana kutoka wastani wa vifo 25 hadi wastani wa vifo saba kwa kila vizazi hai 1,000 na idadi ya rufaa kwenda nje ya nchi nazo zimepungua kwa asilimia 95. (*Makofi*)

Aidha kutokana na kuimarishwa kwa matibabu ya kibingwa, baadhi ya wagonjwa kutoka mataifa jirani wameanza kuja kutibiwa nchini hususan magonjwa ya moyo na hii inadhahirisha kuwa tumefanya kazi kubwa sana katika kuboresha na kuimarisha sekta ya afya nchini. Ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji; tumetekeleza miradi 1,423 ambapo miradi 1,268 ni ya vijiji na miradi 155 ni ya mjini. Miongoni mwa miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa ni wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Nzega, Tabora na Igunga. Mradi wa Maji wa Arusha pamoja na mradi wa kupeleka maji kwenye miji 28 nao unatekelezwa kwa gharama ya shilingi trillioni 1.2. Miradi mingine ya maji ilielezwa

vizuri kwenye hotuba ya Waziri wa Maji wakati akiwasilisha bajeti yake na kutokana na jitihada zilizofanyika, upatikanaji wa maji safi na salama vijiji umeongezeka kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 70.1 mwaka 2020. Na kwa maji mijini nako kumeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeimarisha huduma za mawasiliano hususan kwa kuboresha usikivu wa simu kuutoka asilimia 79 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 94 mwezi Desemba, 2019. Aidha, idadi ya watumiaji wa simu za mkononi pamoja na watumiaji *dataimeongezeka* maradufu na hali hiyo imechangiwa zaidi na kupungua kwa gharama za kupiga simu kwa dakika moja kutoka shilingi 267 kwa mwaka 2015 hadi shilingi 40 tu hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumefanikiwa kufufua shirika letu la simu ya *TTCL*, ambalo lilikuwa limekufa pamoja na kuongeza hisa zetu kwenye kampuni ya *Airtel*/hadi kufikia 49. Huu ni ushahidi mwagine kwamba kazi tuliyotumwa na Watanzania tumeifanya kikamilifu. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbali na kuboresha huduma za jamii, tumetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hususan katika ujenzi, uchukuzi, nishati ya umeme na tumekamilisha ujenzi wa barabara zenyе urefu wa kilometa 3,500 kwa kiwango cha lami na hivyo kuifanya nchi yetu iwe na kilometa takribani 13,000 za barabara za lami. Barabara nyininge zenyе urefu wa zaidi ya kilometa 2,000 zinaendelea kujengwa. (*Makofi*)

Aidha, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu tuemjenga barabara za juu (*flyovers and interchange*) na hizi tumeanza kuzijenga kwa Dar es Salaam ili kupunguza tatizo la msonngamano wa magari na pia tumekamilisha ujenzi wa madaraja makubwa 13 likiwemo Daraja la Nyerere Kigamboni, Daraja la Magufuli kule Mto Kilombero pamoja na Daraja la Sibiti na wakati huo huo ujenzi wa madaraja

mengine makubwa unaendelea likiwemo Daraja la Kigongo – Busisi lenye urefu wa kilometra 3.2; Daraja la Salenda lenye urefu wa kilometra 1.3 pamoja na Daraja la Wami lenye urefu wa mita 513.5. Kwa ujumla kweye awamu hii hakuna Mkoa/ Wilaya ambayo haikupatiwa fedha za kujenga barabara za lami. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Mikoa na baadhi ya Makao Makuu ya Wilaya sasa yameendelea kumeremeta kwa lami na taa za barabarani. Hata wewe Spika ni shahidi, hapa Dodoma miaka mitano iliopita barabara hazikuwa hivi, hata taa za barabarani zinawamulika mpaka watani zangu Wagogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, na ahadi yetu ambayo napenda niitoe ni kuhakikisha tunaiunganisha mikoa kwa barabara za lami na hiyo ahadi inaendelea kutekelezwa kwa asilimia kubwa. Kwa mfano katika Mkoa wa Rukwa, Katavi na Mkoa wa Katavi hadi Tabora na Singida – Tabora, Tabora – Kigoma na Kigoma – Kagera nayo inaendelea kuunganishwa kwa barabara za lami. Nitoe mfano tu, barabara ya Mpanda hadi Tabora yenyе jumla ya kilometra 359 wakandarasi wanne wapo wanaendelea kujenga kwa kiwango cha lami. Ni matumaini yangu Waziri ataendelea kuisimamia hata kama ataenda kuomba kura kule lakini barabara hii lazima ikamilike mapema kwa kiwango cha lami. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, barabara ya Manyoni – Tabora palikuwa pamebaki kilometra 85 kati ya Nyahua na Chaya, lakini naambiwa mkandarasi amebakiza kilometra 27 tu ili barabara hii nayo ikamilike kwa kiwango cha lami. Lakini barabara ya kutoka Mpanda – Kigoma na kutoka Kigoma – Nyakanazi nazo zinaendelea kujengwa kwa kiango cha lami. Ushahidi wanao Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa sababu wanawaona wakandarasi katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nina haki ya kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kusimamia kazi nzuri katika maeneo yao, kwani kazi zao wamezifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kujenga barabara tunakamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro yenye urefu wa kilometa 300 na ujenzi wa awamu ya pili kutoka Morogoro hadi Makutupora umbali wa kilometa 422 umefikia asilimia 30. Miradi hii miwili inagharimu shilingi trillioni 7.062 na fedha zote zinatolewa na Serikali kwa asilimia 100. Ujenzi wa sehemu ya Mwanza - Isaka - Dodoma iko kwenye maandalizi na yenye we ina uhakika hivi karibuni tutaitangaza ili nayo ianze kujengwa na sehemu zingine zitafuatia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumekarabati pia reli za zamani kw amfano kutoka Dar es Salaam hadi Isaka kilometa 970, na hali kadhalika tumeefufua usafiri wa reli ya Dar es Salaam - Tanga - Moshi hadi Arusha ambapo usafiri huu ulisimama kwa takribani miaka 20, lakini katika kipindi cha miaka mitano tumefanikiwa kurudisha tena usafiri. Nina uhakika ndugu zangu Wapare na Wachaga akina *bwashee shininga pesa oshonkorentyani* sasa watafaidi kwa kusafiri kwenye treni na Mheshimiwa Mbatia sasa anaweza akawa anatumia treni kwenda Moshi badala ya kutumia gari. Huu ni uthibitisho kuwa kazi kubwa imefanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa maji, hivi sasa tunafanya upanuzi wa bandari zetu kuu za Da es Salaam, Mtwara na Tanga. Vile vile tumeboresha usafiri wa maji kwenye maziwa yetu makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kwa kuboresha bandari zake pamoja na kujenga na kukarabati meli. Kwenye ziwa Victoria kwa mfano, tumekarabati meli tano, Mv Victoria, Mv Butiama, Mv Clalius, Mv Umoja na Mv Wimbi na tunaendelea na ujenzi wa meli mpya kubwa ya Mv Mwanza Hapa Kazi Tu itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400. Kwenye Ziwa Victoria pia tumejenga cherezo kubwa kuliko zote katika Ziwa Victoria kwa ajili ya kujenga na kukarabati meli. Kwa upande wa Ziwa Tanganyika, tumekartabati meli ya mafuta ya Mv Sangara na tuko mbioni kuanza ukarabati wa Mv Lihembu. Kwenye Ziwa Nyasa tumejenga meli mpya ya kubeba abiria 200 na mizigo tani 200. Jambo la kufurahisha zaidi ni kwamba wenzenetu kule Zanzibar wamenunua meli kubwa mbili kwa ajili

ya kutoa huduma katika Bahari ya Hindi, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Shein na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makof/ Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, katika mipango ya baadaye, tuna mpango wa kujenga meli mpya kwa ajili ya kutoa huduma kati ya Bandari ya Mtwara na nchi ya Comoro na kati ya Bandari ya Kalema na Kalemii nchini DRC. Tunataka magari na mizigo inayosafirishwa kutoka kwenye bandari yetu isihangaike kupita kwenye nchi jirani, iende moja kwa moja mpaka DRC. Nina uhakika tutakuwa tumejenga uchumi wetu mkubwa kwa kuunganisha nchi hizi mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo tumejenga vivuko vipyta na kukarabati vivuko vya zamani vipatavyo 17. Kuhusu usafiri wa anga, tumekamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria (*Terminal III*) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na tunaendelea na upanuzi wa Viwanja vya Kimataifa vya Kilimanjaro na Abeid Amani Karume kule Zanzibar. Vilevile ujenzi wa viwanja vingine 11 upo katika hatua mbalimbali na tuko mbioni pia kumpata mkandarasi wa kujenga kiwanja kikubwa sana hapa Dodoma cha Msalato ambapo fedha zipo. Lakini pia tutajenga barabara ya kilometra 110 ya njia nne inayozunguka hapa hapa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekamilisha pia ujenzi wa rada Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na kule Songwe Mbeya ujenzi wake unakaribia kukamilika. Sambamba na hilo, tumefufua Shirika letu la Ndege la ATCL kwa kununua ndege mpya 11 ambapo ndege nane tayari zimewasili na zile zingine zinaendelea kutengenezwa na hii imeongeza idadi ya wasafiri wa anga nchini kutoka milioni 4.8 mwaka 2015 hadi wasafiri milioni 5.8 mwaka 2018/2019. Faida nyiningine ya kuwa na ndege tumeiona katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona ambapo kwa kutumia ndege zetu tumeweza kuwarejesha Watanzania wenzetu waliokuwa wamekwama nchi mbalimbali ikiwemo India. Kama tusingkuwa na ndege zetu ingekuwa vigumu kuwarejesha Watanzania hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali uimarishaji wa miundombinu ya usafiri, tumeboresha upatikanaji wa nishati ya umeme. Tumekamilisha mradi wa Kinyerezi II ambao umetuongezea megawatts 240 na tunakaribia kukamilisha upanuzi wa mtambo ya Kinyerezi I utakaozalisha megawatts 325 kutoka megawatts 150, lakini muhimu zaidi tumeanza kutekeleza mradi mkubwa wa Bwawa la Nyerere kwenye Bonde la Mto Rufiji. Mradi huu ulipigwa vita sana, lakini tumefanikiwa na gharama ya mradi huu ni trillioni 6.5 na fedha zote zinatolewa na Watanzania. Utakapokamilika mradi huu utazalisha megawatts 2,115 ambazo sio tu zitatuhakikishia umeme wa kutosha na wa gharama nafuu, lakini pia utatusaidia kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira unaosababisha na matumizi mabaya ya kuni na mkaa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kutekeleza miradi mingine kwa kutumia vyanzo mbalimbali ikiwemo maji, gesi asilia, juu, upepo na kadhalika. Aidha, tumekamilisha miradi mikubwa ya kusafirisha umeme ikiwemo mradi wa Iringa – Shinyanga – Makambako, Makambako – Songea, Lindi – Mtwara na kadhalika. Pamoja na kuendelea kutekeleza mradi wa kupeleka umeme vijiji ambapo tumeongeza idadi ya vijiji vilivyo fikishiwa umeme kutoka vijiji 2018 mwaka 2015 hadi vijiji 9,112 mwezi Aprili, 2020. Na nchi yetu ina vijiji 12,268 hivyo tumebakiza vijiji 3,156 tu. tukichaguliwa hatutaweza kushindwa vijiji hivi 3,156 tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua tulizozichukua, idadi ya watumiaji wa umeme (*energy access*) imeongezeka kutoka asilimia 35 hadi asilimia 85 na hii imechagizwa sana na ushushwaji wa gharama za kuanganisha umeme kutoka shilingi 177,000 hadi shilingi 27,000 tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, matukio mengine tuliyoyapata kwenye sekta ya nishati ni kupunguza tatizo la kukatikakatika kwa umeme. Katika kipindi chote cha miaka mitano, nchi yetu haikuwahi kuingia gizani. Zaidi ya hapo tumeokoa kiasi kikubwa cha fedha kwa kuzima mitambo ya kuzalisha umeme

wa mafuta. Kwa mfano kwa kuzima mitambo ya *IPTL*, *AGGREKO* na *Symbion* tumeokoa shilingi bilioni 719 kwa mwaka. Na hii ndiyo imesaidia *TANESCO* sasa ianze kujindesha yenye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati nikizindua Bunge hili nakumbuka niliahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ingeendelea na jitihada za awamu zilizotangulia za kukuza uchumi pamoja na kukabiliana na matatizo ya umaskini na ukosefu wa ajira. Hivyo basi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumejitahidi kwa kiasi kikubwa sana kutekeleza ahadi hiyo hususani kwa kukuza sekta zetu kuu za uchumi na uzalishaji ikiwemo viwanda, kilimo, biashara, madini pamoja na utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, tumejenga viwanda vipyta 8,477 ambapo vikubwa ni viwanda 201, vya kati ni 460, vidogo ni 3,406 na vidogo sana ni 4,410. Hii imeongeza idadi ya viwanda nchini kutoka viwanda 52,633 mwaka 2015 hadi viwanda 61,110 mwaka 2020. Viwanda vipyta vilivyojengwa vimeisaidia kuifanya nchi yetu kujitosheleza kwa baadhi ya bidhaa ikiwemo saruji, nondo na batii. Aidha, viwanda vipyta vimezalisha ajira 482,601. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kujenga viwanda, tumeendelea kuweka mkazo kwenye sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Kama unavyofahamu sekta hii bado ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, inachangia takribani asilimia 25 ya fedha za kigeni, asilimia 30 ya Pato la Taifa, asilimia 65 ya malighafi za viwandani na asilimia 70 ya ajira zote nchini, lakini pia inachangia asilimia 100 ya mahitaji yetu ya chakula. Hivyo basi, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumeendelea kuipa kipaumbele sekta hiyo na tumeongeza upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea, viuatilifu na matrekta. Tumeongeza uzalishaji wa miche ya mazao ya kimkakati, tumejenga na kukarabati skimu za umwagiliaji, vihenge vya kuhifadhi mazao, tumefufua masoko ya mazao, tumetafuta masoko na tumeimarisha vyama vya ushirika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2015 hadi hekta milioni tano mwaka 2020. Na hii imesaidia sana kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji. (*Makof*)

Pia tumejenga mabwawa mapya 104, tumeongeza idadi ya ng'ombe waliohamilishwa kutoka 105,000 mwaka 2015 hadi 514,700 mwaka 2020, tumetoa chanjo ya mifugo na kusambaza dawa za kuingeshea mifugo, tumeimarisha pia ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kuanzisha kanda kuu tatu za Ziwa Victoria, Tanganyika na Pwani pamoja na kudhibiti matumizi ya zana za haramu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kuna wakati Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mpina alikuwa akitembea na rula hadi kwenye migahawa lakini hii illkuwa ni katika kazi ya kuhakikisha tunapata mafanikio haya ambayo tumeyapata. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo tumehamasisha na kufanikiwa kuongeza idadi ya wafugaji samaki kutoka 18,843 mwaka 2015 hadi 26,474 mwaka 2020, tumeongeza idadi ya mabwawa kutoka 22,545 hadi 26,445, vizimba vyta kufugia samaki (*fish cages*) kutoka 109 hadi 431 na uzalishaji wa vifaranga kutoka vifaranga 8,090,000 hadi vifaranga 14,531,487. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo mwaka 2017 tulizindua Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Kilimo (*ASDP II*) wenyе malengo wa kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa, kibashara na chenye tija. Vilevile tumeongeza mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) kwa shilingi bilioni 208 kuitia mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Serikali pia imeipatia *TADB* dola za Marekani milioni 25 sawa na shilingi bilioni 57.8 ili kuendesha Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogowadogo wenyе lengo la kuchagiza mabenki na taasisi za fedha kuongeza utoaji wa mikopo kwa wakulima wadogowadogo na makampuni madogo na ya kati ya kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali imeipa *TADB* shilingi bilioni 324.8 na hivyo kuiwezesha benki hiyo kutoa mikopo ya moja kwa moja kwa wakulima, wafugaji na wavuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 166.9 kwa riba nafuu. Kutokana na hatua hizi, mafanikio makubwa yamepatikana, mathalani uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 15,528,820 mwaka 2015/2016 hadi tani 16,891,974 mwaka 2018/2019. Mahitaji yetu ya chakula kwa mwaka ni chini ya tani milioni 14, kwa upande wa mazao ya biashara uzalishaji umeongezeka kutoka tani 796,502 hadi tani 1,144,163.1. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye uvuvi; sangara kwenye Ziwa Victoria wameongezeka kutoka tani 419,936 mwaka 2016 hadi tani 816,964 mwaka 2020 na urefu wa sangara umeongezeka kutoka wastani wa sentimita 16 hadi sentimita 25.2 na hivyo, samaki wetu kuanza kuhitajika kwa kiasi kikubwa katika soko la Ulaya na ninyi ni mashahidi Waheshimiwa Wabunge ndege zimeanza kuja Mwanza na kubeba samaki wetu kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi. Na kwa kuzingatia hilo, mauzo ya samaki nje ya nchi yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 379 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 692 mwaka 2019; haya siyo mambo madogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kukuza uchumi pia tumeendelea kuboresha mazingira ya biashara na utekelezaji wa nchi ikiwemo kuanza kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira. Na haya mazingira ni mazingira yetu ya biashara nchini kwa kutumia *blueprint* na kuanzisha Wizara maalum ya Uwekezaji iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tumefanya marekebisho ya sheria mbalimbali na kupunguza urasimu katika kutoa vibali na pia kufuta tozo zenye kero 173 ambapo tozo 114 zinahusu sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo na tozo 54 za sekta nyingine mbalimbali na tozo tano zilikuwa zinatozwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo, mafanikio makubwa yamepatikana kwenye nyanja za biashara na

uwekezaji. Biashara yetu nje imeongezeka kutoka shilingi triliuni 11.5 mwaka 2014/2015 hadi kufikia shilingi triliuni 16.6 mwaka 2018/2019. Jambo la kufurahisha zaidi ni kwamba Tanzania imekuwa na ulali chanya wa mauzo ya bidhaa kwenye masoko ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfano, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka mwaka 2015 hadi 2018, Tanzania imekuwa na ulali chanya wa mauzo ya bidhaa kwa wastani wa dola za Marekani millioni 288.04. Na kuhusu uwekezaji, Kituo chetu cha Uwekezaji kimesajili miradi mipya 1,307 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 14 na 607 na zaidi ya shilingi triliuni 30 na itakayopatikana itatoa ajira 183,503. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya madini mageuzi makubwa sana yamefanyika ikiwa ni pamoja na kuanzisha Wizara mahususi ya Madini, kudhibiti utoroshaji na usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi, kuanzisha masoko ya madini kwenye kila mkoa na kuongeza ushiriki wa wafanyabiashara wetu wadogo kwenye myororo wa uchumi wa madini na kuwafutia ama kuwapunguzia viwango vya kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo na muhimu zaidi mwezi Julai 2017 tulipitisha Sheria ya Kulinda Rasilimali za Taifa (*The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act*) ya mwaka 2017 ikiwemo madini, nakushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuitisha sheria hii muhimu sana kwa Taifa letu. Kwa hakika mmeingia kwenye vitabu vya historia ya nchi yetu na ninaamini vizazi hadi vizazi vitawakumbuka kwa kazi hii kubwa mliyofanya chini ya usimamizi wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuitishwa kwa sheria hiyo ndiko kumewezesha kwa mara ya kwanza Watanzania kumiliki rasilimali zao kwa nguvu za kisheria na sheria hiyo pia ndiyo imefanikisha kuanzishwa kwa *Twiga Mineral Company* ambayo Serikali yetu inamiliki hisa asilimia 16 na Kampuni ya

Barrick asilimia 84 na hali kadhalika kutolewa kwa malipo ya fidia ya dola za Marekani milioni 100 kati ya dola milioni 300 ambazo Kampuni ya Barrick ilikubali kutulipa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nikushukuru wewe kwa kuunda Kamati Maalum ya Bunge ya kuchunguza utoroshaji wa madini ya *Tanzanite* ambayo nayo ilitoa ushauri wa kujenga ukuta wa kilometa 25 katika Mgodi wa Mererani ambao sisi Serikali kwa sababu ni wasikivu tuluijenga kwa haraka sana. Kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa, sekta ya madini sasa imeanza kukua kwa kasi kubwa ambapo mwaka 2019 ilongoza kwa ukuaji kwa asilimia 17.7 ikifuatiwa na ujenzi kwa asilimia 14.1. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, mapato yatokanayo na madini nayo yameongezeka, mathalani kwenye mwaka wa fedha 2018/2019 zillikusanya shilingi bilioni 346 kutoka shilingi bilioni 194 mwaka 2016/2017. Kwenye mwaka huu wa fedha wa 2019/2020 tunatarajia kukusanya shilingi bilioni 470 ambapo mwezi wa Aprili, 2020 pekee licha ya kuwepo kwa tatizo la ugonjwa wa Corona, tumekusanya shilingi bilioni 58; haijawahi kutokea kiwango cha juu kabisa tulichowahi kukusanya kwa mwezi ilikuwa shilingi bilioni 43. Haya yametokana na kupitishwa kwa sheria mliyopitisha ninyi Waheshimiwa Wabunge, hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine tuliyoyapata kwenye sekta ya madini ni kutolewa kwa leseni 221 za uchenjuaji madini, leseni nne za uyeyushaji madini (*smelting*) na leseni nne za usafirishaji madini (*refining*). Vilevile tumetenga hekta 38,567 kwa ajili ya wachimbaji wadogwadogo na kuwapatia mafunzo wachimbaji wadogowadogo 10,338. Kwa ujumla hivi sasa wachimbaji wadogowadogo hawabughudhiwi. Mtakumbuka zamanii wachimbaji wadogowadogo waliendesha shughuli zao kama wakimbizi, sisi tukasema hatutaki kuona wananchi wetu wakiwa wakimbizi ndani ya Taifa lao. Na kweli kwa hatua tulizochukua, tumeweza kujenga heshima kwa wananchi kwa kuwawezesha kutengeneza maisha yao bila bughudha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii tumechukua hatua mbalimbali za kukuza sekta hiyo ikiwemo kuanza kutekeleza mpango wa utekelezaji wa utalii Nyanda za Kusini, kuanzisha hifadhi mpya tano; Hifadhi ya Nyerere, Hifadhi ya Chato Burigi, Hifadhi ya Ibanda Kyerwa, Rumanyika na Karagwe na kuongeza jitihada za kutangaza vivutio tulivyonyavyo kimataifa ikiwemo kuanzisha *channel* maalum ya utalii ya *Television* ya Taifa.

Aidha, kama tulivyoahidi tumezidisha mapambano dhidi ya ujangili kwa kuanzisha Jeshi Usu na hivyo kusaidia kuongezeka kwa idadi ya wanyama waliokuwa kwenye hatari ya kutoweka kama vile faru na tembo. Mathalani idadi ya faru imeongezeka kutoka 162 mwaka 215 hadi 190 mwaka 2019. Tembo nao wameongezeka kutoka 43,330 mwaka 2014 hadi tembo 51,299 mwaka 2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo idadi ya watalii na mapato yameongezeka kwa mfano mwaka 2019 tulipokea watalii 1,510,151 kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015. Aidha, mapato yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.9 mwaka 2015 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019. Kama isingekuwa tatizo la kuibuka kwa janga la Corona naamini mwaka huu pia idadi ya watalii na mapato yake yangeongezeka maradufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta nyingine ambayo haijasemwa sana lakini kwa sasa ina mchango mkubwa kwenye uchumi wetu ni sanaa na utamaduni. Kwa mujibu wa taarifa za hali ya uchumi ya mwaka 2018 shughuli za sanaa na burudani ziliongoza kwa ukuaji mwaka 2018 ambapo sekta hii ilikua kwa 13.7% na kwa mwaka 2019 ilishika nafasi ya tatu kwa ukuaji wa asilimia 11.2, hongereni sana wasanii wetu mbalimbali hususan wa bongo fleva, filamu, michezo mbalimbali mpira na kadhalika, kazi zenu siyo tu zinaburudisha na kuchangia ukuaji uchumi, lakini pia zinaitangaza nchi yetu kimataifa na katika hilo naipongeza sana Timu yetu ya Taifa ya Soka ambayo baada ya takriban miaka 39 kupita hatimaye mwaka jana wa 2019 ilifanikiwa kufuzu kushiriki fainali za Kombe la Afrika. (*Makofi/Vigegele*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia wanamichezo mingine waliopeperusha vyema bendera yetu katika miaka mitano iliyopita hususan katika ndondi na riadha. Kutokana na mchango mkubwa unaotolewa na wasanii na wanamichezo nchini Serikali imejipanga katika miaka mitano ijayo kuweka mkazo mkubwa zaidi kwenye sekta hii ambayo ni sekta iliyoajiri vijana wetu wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sekta nyingine tulizoshughulika na kutoa mchango kwenye ukuaji wa uchumi ni pamoja na ulinzi, sayansi na teknolojia, habari, misitu, ufugaji nyuki, mazingira na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye ulinzi mathalani tumeviimarisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ikiwepo Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi, Idara ya Usalama, Magereza, Uhamilaji, Zimamoto, TAKUKURU, Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevyaa kwa kuvipatia vifaa na zana za kisasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sayansi na teknolojia tumeanzisha vituo mahiri vya mafunzo kwa taasisi za elimu ili kuzalisha vijana wenyewe uwezo unaohitajika kitaifa, kikanda na Kimataifa kwa gharama ya dola za Marekani milioni 75. Taasisi hizo ni Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, itakayobobeaa katika TEHAMA na Taasisi ya Teknolojia ya Mwanza itakayobobeaa kwenye masuala ya ngozi Chuo cha Taifa ya Usafirishaji kitakachobobeaa katika taaluma ya anga na Chuo cha Ufundi Arusha kitakachobobeaa katika nishati. Kwa sababu ya ufinyu wa muda sitaweza kuzieleza sekta zote itoshe tu kusema Serikali imejitahidi kuimarisha sekta zote ili kukuza uchumi nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua tulizochukua za kuimarisha sekta mbalimbali kiuchumi wa nchi yetu umeendelea kukua vizuri ambapo kwa wastani katika miaka mitano iliyopita uchumi wetu umekua kwa 6.9% kutoka ukuaji wa 6.2% mwaka 2015. Pato ghafi la Taifa limeongezeka kutoka shilingi triliioni 94.349 mwaka 2015 hadi kufikia shilingi triliioni 139.9 mwaka 2019 na hii ni kulingana na bei ya miaka

husika (*current prices*) hii siyo tu imetufanya tuwe miongoni mwa nchi zinazokuwa kwa kasi kiuchumi lakini imeifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 zenye uchumi mkubwa zaidi Barani Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumefanikiwa pia kudhibiti mfumuko wa bei kutoka 6.1% mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa 4.4% sambamba na hilo akiba ya fedha za kigeniimeongezeka kutoka dola za Marekani milioni 4.4 zilizokuwa zikitosheleza kununua bidhaa na huduma kwa miezi 4.3 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 5.3 kwa mwezi Aprili, 2020 ambazo zinatosheleza kununua bidhaa na huduma kwa miezi 6.2; kiwango hiki ni zaidi ya lengo lilllowekwa kwenye *East Africa Community* ambaao ni miezi 4.5 na ni zaidi ya lengo lilllowekwa na nchi za *SADC* ambaao ni miezi sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapambano dhidi ya umaskini, umaskini wa kipato umepungua hadi kufikia 26.4% mwaka 2017/2018 na kwa lengo la kuendelea kupambana na umaskini mwezi Februari, 2020 tumezindua kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya mpango ya kunusuru kaya maskini - *TASAF* ambaao utagharimu shilingi trillioni 2.032. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukabiliana na tatizo la ajira kupitia jitihada zilizofanyika ikiwemo utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo nisingependa kuitaja hapa, tumefanikiwa kutengeneza ajira zipatazo 6,032,299. Kati ya ajira hizo 1,975,723 zimezalishwa na sekta rasmi na ajira 4,056,576 zimezalishwa na sekta isiyo rasmi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ambayo tumeyapata ni kwenye nyanja za sheria na utoaji haki katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Katika nyanja ya sheria tumejitahidi sana kupunguza vitendo vya rushwa, ucheleweshaji na ubambikaji wa kesi pamoja na tatizo la mlundikano wa wafungwa. Mathalani ili kukabiliana na tatizo la ucheleweshaji wa kesi Serikali iliteua Majaji 17 wa Mahakama ya Rufani na Majaji 52 wa Mahakama Kuu na

kuajiri watumishi wa mahakama 859 wakiwemo Mahakimu 396. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, tumejenga Mahakama Kuu mpya mbili kwa Mkoa wa Mara na Kigoma na kukarabati nyingine nne katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Shinyanga, Sumbawanga na tumejenga pia Mahakama za Hakimu Mkazi tano, Mahakama za Wilaya 15 pamoja na Mahakama za Mwanzo 18 na hali kadhalika tumeanzisha Mahakama za Kutembea (*Mobile Court*) ambayo imeanza kufanyakazi kwenye mikoa ya Dar es Salaam pamoja na Mwanza na mpaka mwezi Machi 2020 ilishasajili mashauri 337 na kusikiliza mashauri 274. Nampongeza sana Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kazi kubwa na naipongeza pia mahakama kwa kuchukua hatua za kupunguza mlundikano wa kesi ikiwemo kuimarisha matumizi ya TEHAMA ambayo siyo tu imeharakisha uendeshaji wa mashauri lakini pia imepunguza tatizo la rushwa kwa watumishi wa mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika jitihada za kukabiliana na tatizo la ucheleweshaji wa kesi nilisaini hati ya kuimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkoo na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na pia kuanzisha Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali. Uwekaji saini hati hiyo umeongeza tija na kuleta ufanisi mkubwa katika usimamizi na uendeshaji wa mashauri mahakamani na pia kwenye mabaraza ya usuluhishi ndani na nje ya nchi. Zaidi ya hapo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumewasamehe wafungwa 42,774 waliokuwa wakitumikia vifungo mbalimbali na hivyo kupunguza mlundikano magerezani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, katika zoezi la ukaguzi na kusikiliza changamoto za wafungwa na mahabusu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imewafutia kesi mahabusu 2,812. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jaji Mkoo Profesa Juma, Mheshimiwa Jaji Kiongozi Ndugu Felesh, Waheshimiwa Majaji wengine, Mahakimu, Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Mkurugenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na Wakili

Mkuu wa Serikali kwa kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini ambao umesaidia mafanikio haya makubwa. Pia nawashukuru watumishi wote wa mahakama na Ofisi ya AG kwa kazi nzuri bila kumsahau AG ambaye pia ni Mbunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumeshughulikia pia kero mbalimbali za wananchi hususan wakulima, wavuvi, wafugaji, wafanyabiashara, wafanyakazi, wajasiriamali na bila kusahau migogoro ya ardhi. Kwa upande wa wakulima, wavuvi, wafugaji na wafanyabiashara kama nilivyosema awali tumefuta takribani tozo 114 tozo hizi zilikuwa zikikwamisha shughuli zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa wafanyakazi tayari nimeshaeleza kuhusu upandishaji vyeo na malipo ya madeni mbalimbali. Zaidi ya hapo tumeponguzza kodi ya mapato kutoka 11% hadi 9% na kulipa deni la shilingi trillioni 1.2 ambalo Serikali ilikuwa ikidaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hivyo kuwezesha wastaifu kuendelea kulipwa mafao yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wajasiriamali wadogo wakiwemo wamachinga, mamalishe, waendesha bodaboda na bajaj tumejitahidi kuwawekea utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli zao bila kubughudhiwa na kupatiwa vitambulisho maalum vilivytotolewa kwa gharama nafuu. Mwaka jana 2019 jumla ya wajasiriamali wadogo 1,591,085 walipatiwa vitambulisho hivyo na hivyo kuwafanya waondokane na usumbufu uliokuwepo. Mtakumbuka zamani kabla ya utaratibu huo kuanza wajasiriamali wadogo wadogo walikuwa wakibughudhiwa sana hasa mgambo ikiwemo kuwanyang'anya mali zao hivyo kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa vitambulisho hivyo tumedhihirisha kuwa Serikali ya Awamu ya Tano iko kwa ajili ya wanyonge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kutoa vitambulisho kwa wajasiriamali wadogo tumetunga sheria yenye kuzitaka Halmashauri zote kutenga 10% ya mapato yao kwaajili ya kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanawake 4%, vijana 4% na

walemavu 2% ambapo hadi mwezi Machi kiasi cha shilingi biliioni 93.2 kilikuwa kimeshatolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kero nyingine tulioshughulikia ni ya migogoro ya ardhi baadhi ya hatua tulizochukua ni kuanzisha Ofisi ya Ardhi kwenye mikoa yote ambayo sasa huduma zote za upangaji, upimaji, umilikishaji na uthamini pamoja na usajili wa hati, nyaraka na ramani na michoro zinapatikana katika mikoa husika. Hii imeongeza kasi ya urasimishaji makazi ya wananchi na pia utoaji hati. Jumla ya maeneo ya viwanja yaliyorasimishwa ni 764,158 na tumetoa hati miliki za kimila 515,474 na kubwa zaidi ni uamuvi ulifanywa na Serikali wa kuvirasimisha vijiji 920 kati ya vijiji 975 vilivyokuwa kwenye maeneo ya hifadhi. Hii imesaidia sana wananchi waliokuwa wanaishi kwenye maeneo ya hifadhi sasa waishi salama kwa raha kwa kufanyakazi zao na kurasimishwa kwa vijiji 920 imesaidia kuondoa migogoro kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumeimarisha pia uhusiano na ushirikiano na mataifa ya nje pamoja na taasisi za kimataifa. Hii ndiyo sababu tuliweza kuwapokea viongozi wa nchi na taasisi mbalimbali za kimataifa ikiwemo Vietnam, India, Uturuki, Afrika Kusini, DRC, Ethiopia, Misri, Rwanda, Zambia, Zimbabwe, Uganda, IMF, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, IFAD na kadhalika. Katika kipindi hicho pia tumefungua Balozi mpya nane; Balozi hizo ni Algeria, Cuba, Israel, Korea, Qatar, Namibia, Sudan na Uturuki. Aidha, nchi mbili Ethiopia na Poland nazo zimefungua Balozi zao hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo tunaendelea kushiriki katika shughuli na mipango mbalimbali ya kimataifa ikiwemo ulinzi wa amani ambapo kwa sasa tuna askari wapatao 2,303 katika nchi ya DRC, Jumuuya ya Afrika ya Kat, Lebanon na Sudan Kusini. Zaidi ya hapo nchi yetu imeaminiwa kuongoza jumuuya mbili za kikanda Jumuuya ya Afrika Mashariki kuanzia 2016 hadi 2017 na pia kuongoza SADC kuanzia mwezi Agosti, 2019 hadi mwezi Agosti, 2020. Pamoja na mafanikio tuliyopata katika kuongoza taasisi hizo ni kuzishawishi pia nchi wanachama kuridhia lugha ya

Kiswahili kutumika kwenye taasisi hizo. Haya yote ni mafanikio tuliyoyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 151(c) ya llani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015 na 2020 Chama cha Mapinduzi kiliahidhi na ninapenda kunukuu; "Kusimamia azma ya Serikali kuhakikisha majengo yote ya Wizara za Serikali yanajengwa Dodoma balada ya Dar es Salaam." Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kubwa kulialifu Bunge lako tukufu kuwa ahadi hiyo tumeitekeleza na tumeitekeleza siyo tu kwamba majengo ya Wizara zote yamejengwa Dodoma bali Serikali yote tayari imeshahamia Dodoma ambapo tarehe 13 Aprili, 2019 nilizindua Mji wa Serikali pale Mtumba. Hii ina maana kuwa tumetekeleza ahadi yetu zaidi ya tulivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, nina imani kwa kutekeleza ndoto hiyo iyodumu kwa miaka 47 na siyo tu tumemuenzi Baba wa Taifa lakini pia Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Halmashauri wa *TANU* uliofanya uamuzi wa kuihamishia Makao Makuu nchi yetu... (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Yajayoo....

WABUNGE FULANI: Yanafurahisha. (*Makofi*)

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, uamuzi huu ulifanyika mwaka 1973 hivyo naamini utanisamehe nikisema kwa mbali CCM oyeee.

WABUNGE FULANI: Oyeeeeee. (*Makofi/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: CCM, CCM. (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, ahsanteni Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nachomekea tu hapa, lakini kwa kifupi sana haya ni baadhi ya mafanikio tuliyyopapa, lakini kama nilivyo sema awali tumefanya mengi sana ambayo kama ningeamua kuya eleza yote hapa tunaweza kukesha. (*Makofii*)

Kwa bahati nzuri Watanzania wengi wameona na wanayajua. Hivyo nina imani kubwa kwamba Watanzania watandelea kutuamini na kutupa dhamana kuongoza nchi yetu katika vipindi vingine vijavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, binafsi na ammini kutokana na misingi imara tuliyyoweka ya ukuaji uchumi pamoja na uzoefu mkubwa tulipata endapo wananchi wataendelea kutuamini na kutuchangua kuongoza nchi yetu katika miaka mitano ijayo tutafanya mambo mengine makubwa zaidi. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, na tukapoyafanya hayo mambo mengine tutakuwa tumetimiza ndoto na dhamira yetu ya kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati yenye kuongozwa na viwanda pamoja na huduma za jamii ifikapo mwaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana zilijitokeza pia baadhi ya changamoto. Kama ujuavyo hapa duniani sio rahisi kufanya jambo lisikumbane na changamoto ama vikwanzo. Hivyo basi na sisi pia katika miaka hii mitano tume kumbana na changamoto zingine kubwa zingine ndogo ndogo lakini kuwa zaidi ni kuibuka kwa ugonjwa wa Homa ya Mapafu uliosababishwa na virusi wa Corona.

Napenda nitumie fursa hii kulishukuru sana Bunge hili tukufu kwa kuitisha Azimio la kunipongeza, japo ukweli pongezi hizo zinastahili Watanzania wote. Lakini pia pongezi hizo zinastahili Bunge hili kwani pamoja na hofu kubwa ili yokuwepo na ili yokuwepo na imetawala Bunge hili liliendelea na vikao vyake kama kawaida. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili kuendelea na vikao vyake kama kawaida kwa lengo la kuwatumikia Watanzania ingawa nafahamu wapo wachache walokimbia na sijui kama wamesharejea, lakini nisema tu kwamba kukimbia halikuwa ni jambo sahihi kwa sababu matatizo au changamoto hazikimbiwi. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: Kweli.

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, kukimbia changamoto ni ishara ya udhaifu. (*Makofi/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: Kweli.

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, lakini pia ni ishara ya woga, lakini pia ni ishara ya kutokujamini. Siku zote njia sahihi ya kukabiliana na matatizo ni kukabiliana nayo. (*Makofi/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: Kweli.

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, na ndiyo sababu sisi tuliamua kukabiliana na ugonjwa Corona huku tukiwa tumemtanguliza Mwenyenzi Mungu na kwa kufanya hivyo tumeweza mpaka sasa hivi kutatua kwa kiasi kikubwa sio tu kufanikiwa kushinda ugonjwa huo, lakini pia kupunguza athari zake zikiwemo athari za kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu Benki ya Dunia pamoja na Shirika la Fedha Duniani yamebashiri kwamba asilimia 60 ya nchi za Afrika zilizopo Kusini mwa Jangwa Sahara zitashuhuhudia ukuaji hasi yaani *negative* wa uchumi mwaka 2020. Hata hivyo sisi Tanzania kutokana na hatua tulizochukua uchumi wetu hautakua kwa *negative*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaendelea kukua vizuri angalau kwa asilimia 5.5 au zaidi. Zaidi ya hapa tumeweza kulinda ajira za wananchi wetu na tuna uhakika wa usalama wa chakula na pia tumeweza kuendelea na utekelezaji wa miradi yetu mikubwa na hii inadhihirisha kuwa maamuzi yetu yalikuwa sahihi na maamuzi ya Bunge hili kuendelea na vikao nayo yalikuwa sahihi sana. Hongereni sana Spika, hongereni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kwa mara nyingine ndugu zangu kurudia kumshukuru mwenyenzi Mungu kwa kuliepusha taifa letu dhidi ya ugonjwa wa Corona.

WABUNGE FULANI: Amina.

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, na ninawashukuru pia viongozi wa dini na bahati nzuri nimewaona hapa Maaskofu, Wachungaji, Mufti wa Tanzania, na wa madhebehu yote kwa kutikia wito wa Serikali wa kufanya maombi maalumu ya kumuomba Mwenyenzi Mungu kutuepusha na janga la Corona. Najua palipo na Mungu hakuna linaloshindikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru na kuwapongeza pia madaktari na wauguzi wetu kwa kazi kubwa na nzuri na kwa namna ya pekee nampongeza mwana mama jasiri Waziri wa Afya Mama Ummy Mwalimu, kwa uvumilivu wake. (*Makof/Vigelegele*)

Nataka niseme kwa dhati nilimtesa sana Waziri huyu kwa sababu simu nilikuwa nampigia mara nyingi, saa nyingine saa nane usiku, naomba aniombee msamaha kwa mume wake. (*Makof/Vigelegele/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kamati zake zote kwa jinsi walivyosimamia hili. Nataka niwaeleze ninayosema ni ya dhati wamefanya kazi kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninawashukuru sana vyombo vya ulinzi na usalama na viongozi wenzangu ndani ya Serikali lakini nawashukuru pia Watanzania kwa jinsi tulivyosimama pamoja kwa kumtanguliza Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na ugonjwa wa Corana nchini kuendelea vizuri na kwa kweli imepungua sana, napenda nitumie nafasi hii kuanzia tarehe 29 Juni, 2020 nafikiri itakuwa Jumatatu shule zote zifunguliewe zilizokuwa zimebaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini shughuli zingine zote ambazo tulizizua watu kufunga ndoa tumeachelewasha watu kuoana wakati...(*Makofi/Kicheko*)

...nazo ziendelee. maisha ni lazima yarudi kama ilivyokuwa zamani. Hata hivyo naendelea kuwasihililiani Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari na pia kuzingatia ushauri unaotolewa na wataalam wetu wa afya kwa sababu ni muhimu kuzingatia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu napenda nirudie kuwashukuru Watanzania wote wa makundi yote wakiwemo wakulima, wafanyakazi, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara kwa kuiunga mkono Serikali yetu hususani kwa kudumisha amani na mshikamano pamoja nakuchapa kazi kwa bidii. Lakini pia kwa kulipa kodi, lakini pia kwa kuwa tayari kufunga mkanda ili kujenga Tanzania mpya. (*Makofi*)

Nawashukuru sana viongozi wenzangu wote wa Serikali tulioshirikiana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Namshukuru sana Makamu wa Rais mwana mama shupavu na jasiri Mama Samia Suluhu Hassan kwa kunisaidia sana majukumu. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia namshukuru Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushauri na ushirikiano alionipa. (*Makofi/Vigelegele*)

Namshukuru na kumpongeza pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa heshima na unyenyekevu wake, uchapakazi wake mzuri na kutanguliza mbele maslahi ya Taifa. Amenisaidia sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Aidha namshukur makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Idd pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi Mheshimiwa Balozi John Kijazi kwa kufanya kazi kwa bidii bila kuchoka. (*Makofi/Vigelegele*)

Vilevile nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wangu, watu hawa wamefanya kazi usiku na mchana kwa upendo mkubwa sana, walinivumilia sana, hawakuwa na uhakika na Uwaziri wao, lakini wamechapa kazi sana, sana, sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Wilaya zote na Wakurugenzi wa Manispaa na Majiji, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata na Vijiji, Waheshimiwa Mabalozi wa Nyumba Kumi Kumi na watumishi wote wa Serikali kwa kufanikisha kupatikana mafanikio yote niliyoyataja. Kwa ujumla wao wote wamenisaidia sana kwenye kufanya kazi hii. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Shein anamaliza muhula wake na hii ni kwa mujibu wa Katiba. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa utumishi uliotukuka akiwa Makamu wa Rais kwa miaka nane na akiwa Rais wa Zanzibar kwa miaka kumi. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Rais Dkt. Shein kazi umeifanya, ameweka historia ya namna yake katika utumishi wa umma na ametoa mchango mkubwa kwenye Taifa letu. Hivyo basi sasa anapokwenda kupumzika namtakia kila kheri na tuna muahidi kuendelea kumuenzi kama tunavyowaenzi viongozi wengine wastaifu. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nakishukuru pia chama changu CCM kwa kusimamia vizuri Serikali na kuhakikisha llani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 hadi 2020 inatekelezwa vizuri. usimamizi mzuri uliofanywa na CCM kwa Serikali katika miaka hii mitano umethibitisha maneno yaliyowahi kutamkwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere kwamba chamba legelege huzaa Serikali legelege na chama kikiwa imara Serikali nayo huwa imara. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, navishukuru vyama vingine nya siasa ambavyo vilitoa ushirikiano mkubwa kwa Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kama mnavyofahamu wapi baadhi viongozi wa vyama nya siasa ambao licha ya tofauti zetu za kiitikadi walikuwa pamoja na Serikali wakati wote. Nihwashukuru kwa michango yao mizuri, hata hivyo kusema kweli ndivyo inatakiwa iwe kuwa sisi zote ni wamoja na tunajenga Taifa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, niwashukuru sana wana habari kwa kazi kubwa na nzuri waliyofanya ya kuhabarisha na kuelimisha umma wa Tanzania pamoja na dunia nzima kwa ujumla kuhusu masuala mbalimbali ya nchi yetu hususani mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii tuliyoyapata katika kipindi hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine narudia kulishukuru Bunge hili kwa ushirikiano mkubwa uliota kwa Serikali katika kipindi cha miaka mitano, mbali na kushauri na kuisimamia Serikali, Bunge hilo ndilo lilitokuwa kilipitisha bajeti na miswada mbalimbali ya Serikali. Kwa namna ya pekee kabisa nawashukuru Wabunge wa chama changu. (*Makofii/Vigelegele*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Tuna imani na Magufuli

WABUNGE FULANI: Oyaa Oyaa.

MHE. MARTHA M. MLATA: Tuna imani na Magufuli

WABUNGE FULANI: Oyaa Oyaa.

MHE. MARTHA M. MLATA: Magufuli kweli.

WABUNGE FULANI: Kweli kweli kweli.

MHE. MARTHA M. MLATA: Magufuli kweli, kweli...

WABUNGE FULANI: Kweli kweli kweli Magufuli. (*Makofi*)

MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI – RAIS WA JAMHURI YA MIUNGANO WA TANZANIA: Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wabunge wa chama changu kwa kuiunga mkono Serikali yake na kusema kweli mmethibitisha ule usemi usemao uchungu wa mwana aujuaye mzazi. (*Makofi*)

Nawashukuru pia Wabunge wa vyama vingine kwa ushirikiano wao, japo walikuwepo baadhi ambao wenyewe kila jambo wallkuwa wakipinga, lakini nao ninawashukuru, naamini wakati ujao watakuwa wamejifunza kwamba kupinga pinga kila kitu siyo kizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu nawashukuru sana washirika na wadau wengine mbalimbali wa maendeleo kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia, natambua kuwepo wawakilishi pamoja na Mabalozi hapa, ushirikiano wao ulitupa nguvu na ari ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hivyo basi tunawashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao kwa bahati nzuri, wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Serikali aliwatajaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tupo leo hapa na mwanzoni mwa hotuba yangu nilieleza kwamba nimekuja kulihutubia Bunge hili la Kumi na Moja kwa mara ya mwisho. Lakini kabla ya kusahau wa kushukuru na mimi namshukuru mke wangu Janeth Magufuli, pamoja na familia. (*Makofi*)

Ninawaomba muendelee kumuombea mama yangu ambaye amekaa na kiharusi hawezi akazungumza, hawezi akajigeuza, hawezi akala, anakula kwa kutumia mpira kwa

zaidi ya miaka karibu miwili sasa, lakini haya yote ni mapenzi ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, nimekuja hapa kwa ajili ya kutimiza lengo lilioko la Kikatiba na hasa la kuruhusu kuanza kwa mchakato wa uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani utakaofanyika mwezi Oktoba, 2020. Nyote mnafahamu uchaguzi ni zoezi muhimu katika kukuza demokrasia katika nchi yoyote, mbali na kuwapa wananchi fursa ya kuwachagua viongozi wanaowataka, inatoa pia nafasi kwa viongozi kujua endapo bado wanaaminiwa na wananchi na katika hilo natambua kuwa baadhi yenu hapa mmeshaonesha nia ya kuwania tena na wapo walotangaza kutowania tena, nawatakia maisha mema wale walotangaza kustaa fu na ninawatakia kila la kheri wale wanaowania tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini wengi wenu hasa wale wenye kuvali nguo za kijani watarejea, lakini kwa wale ambao hawatabahati kurejea tunawashukuru kwa mchango wao kwenye Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikuthibitishie Bunge hili limefanya kazi kubwa sana na ni Bunge la mfano, haya mafanikio yote tunayoyazungumza kamwe yasingewezekana bila ya kuwa na Bunge mahiri kama hili Bunge la Kumi na Moja. Michango mikubwa iliyopatikana, maendeleo makubwa yaliyopatikana ni kwa sababu ya Bunge hili. Kwangu mimi chini ya uongozi wako nimejifunza mengi kuhusu Bunge hili . (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali kuhusu uchaguzi tumejipanga kuhakikisha uchaguzi wa mwaka huu kama ulivyokuwa chaguzi zilizopita unakuwa huru na haki, tutasimamia uhuru na haki wa vyama vyote na hii ndiyo demokrasia ya kweli. Kwa sababu hiyo navisihivya vyama vyasiasa na wanasiasa kuijandaa vizuri kushiriki katika uchaguzi huu. Navihimiza pia vyama kutoa fursa ya kutosha kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, nawasihi wagombea kuepuka matusi na vurugu, nchi hii ni yetu, nchi

yetu ya Tanzania ni yetu sisi wote, tujiepushe sana na shetani wa matusi, tumtangulize Mungu katika kampeni zetu, matusi na kejeli hayajengi, sisi sote ni wamoja, hivyo tukabishane kwa hoja na kushindanisha ilani zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwa ye yeyote atakayetaka kuleta vurugu namtahadharisha kwamba Serikali iko macho, uchaguzi haumaanishi kuwa Serikali imeenda kulala, Serikali itaendelea kuwepo kusimamia sheria na taratibu za nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu na Waheshimiwa Wabunge nimejithidi kueleza kwa ufupi. Mengi mnayajua ninyi Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kama ni miradi yote mnaijua nilikuwa namsikiliza Silinde leo, anazungumzia juu ya madaraja yake kule na vituo vyake vyaya afya, nikamuona kumbe Silinde ameutambua ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kusema kila Mbunge aliye po hapa awe wa Chama Tawala, wale wa vyama vile vingine vyaya upinzani kila mmoja wao alitimiza wajibu wake kwa ajili ya Taifa hili. Tumeijenga Taifa letu, tumeijenga Tanzania, mafanikio yaliyopatikana ni kwa sababu kila mmoja wakiwepo Watanzania tunaowaongoza walitimiza wajibu wao. Tukaendelee kuisimamia Tanzania yetu, mafanikio haya tumeyapata sisi wote. Mimi ni kiongozi wenu, lakini ninaamini mafanikio haya yamepatikana kwa sababu Watanzania wameyafanya yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena kumshukuru Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu kuwa tulivu, yenye amani na yenye maendeleo makubwa ambayo hayana mfano wake. Tukaendelee kuujenga uzalendo wetu ili kipindi hiki cha uchaguzi kikaishe salama, tukiwa bado tunaupeleka Utanzania wetu mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa natamka kuwa Bunge hili linavunjwa rasmi na tarehe itatangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwatakie mafanikio mema na nataka niwahakikishie zile *t-shirts* zenu zilanza kuingia saa nane za usiku, kwa kila mmoja kwa ajili ya haki na kuzingatia sheria za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Jaji Zanzibar Ndugu Makungu, Wenyeviti wa Bunge hapa ambao mmeefanya kazi nzuri, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Spika wa Zanzibar, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Zanzibar, Waheshimiwa viongozi wastaafu wote mlioko hapa, Waheshimiwa viongozi wa dini, viongozi wa vyombo vyaa ulinzi na usalama na wote waliomo kwenye ukumbi huu na Watanzania wote wanaonisikiliza, kwa heshima kubwa nimefurahi sana kwa kupata nafasi hii, nitaikumbuka katika maisha yangu na kwa unyenyekevu mkubwa napenda niseme ndugu zangu ninawapenda sana, na kwa hili basi nasema Mungu libariki Bunge la Tanzania, Mungu wabariki Wabunge wote, Mungu ibariki Tanzania, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi/Vigelegele*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu, naomba tumpe zawadi ya makofi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Rais ameturasimishia kwamba mwisho wa safari ndiyo hii, pia ametuambia ndiyo mwanzo wa safari nyingine na mimi niwatakie kila la kheri kila mmoja wetu. Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkinituma kila wakati, mwambie na mimi nikamwambia kuhusu utaratibu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niwashukuru, nimshukuru Mheshimiwa Rais mbele yenu kuhusu utaratibu na ametunong'oneza hata mlivokaa hapo utaratibu unaendelea, na utaratibu ni mzuri sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, makofi haya hayatoshi, asiyepiga makofi mchawi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, basi naomba sasa tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki .*(Makof)*

WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)

SPIKA: Naomba tukae Waheshimiwa Wabunge na wageni wetu pia.

Mheshimiwa Rais na wageni wetu wote naomba nichukue nafasi hii kuwatambulisha baadhi ya wageni wetu waliojunga na sisi leo na niwashukuru sana nyote kwa kuitikia mwallko wetu na hasa viongozi wakuu wa Serikali.

Naomba niwatambulishhe wawakilishi wa Vyama vyaa Siasa vyenye usajili wa kudumu kwenye *gallery* popote pale mlipo, ahsanteni sana, ahsanteni sana, tunashukuru sana kwa kufika kwenu, ahsante sana. *(Makof)*

Kwa upande wa Viongozi wa Dini naomba niwatambulishhe Kiongozi wa Dhehebu la Mabohora Tanzania - Hinduism Ndugu Azim Dewji karibu sana, karibu sana yupo pale juu. Mwenyekiti wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania Askofu Peter Konki, ahsante Baba Askofu. *(Makof)*

Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (*TEC*) Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, ahsante sana. *(Makof)*

Mwenyekiti wa *CCT* Dkt. Alinikisye Cheyo, ahsante sana mtani wangu. Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Shehe Mustafa Rajabu, ahsante sana na Mufti Mkuu wa Tanzania Bara Sheikh Aboubakar Zuberi, ahsante sana. *(Makof)*

Mheshimiwa Rais, pia tunao Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma, wakiwakilisha Wakuu wa Wilaya wenzao

wote nchi nzima. Tunaye Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa Jabir Shekimweri, karibu sana; Mkuu wa Wilaya ya Chemba Simon Odunga, ahsante sana; Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Vumilia Nyamonga, ahsante sana na Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Fezalia Makota.

Tunaye pia *DC* wa Bahi Mwanahamisi Mkunda, huyu *DC* wa Bahi alikuwa mtumishi wetu hapa Bunge, alikuwa Katibu wa Kamati ya Nishati na Madini. Tunashukuru Mheshimiwa Rais kuwakumbuka baadhi ya watumishi wetu wa Bunge. Mheshimiwa Rais na tunao wengine wana sifa kemkem, uwe unawakumbuka kumbuka huko Mheshimiwa. (*Makofi*)

Pia tunaye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini Patrobas Katambi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pia tuna Wakuu wa Mashirika ya Umma, Vyuo Vikuu na Taasisi za Fedha wote kwa pamoja.

WABUNGE FULANI: Kongwa, Kongwa.

SPIKA: Wakuu wa Mashirika ya Umma, Vyuo Vikuu na Taasisi za Fedha, ahsanteni sana kwa kufika. (*Makofi*)

Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara za Serikali kwa pamoja ahsanteni sana kwa kufika; Wabunge wa Bunge letu la Afrika Mashariki wakiongozwa na Alhaji Adam Kimbisa, ahsanteni sana, ahsanteni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya kule kwenye Bunge la Afrika Mashariki, tunawashukuruni sana. Jumla yao huwa ni tisa lakini kwa sababu kuna vikao vinavyoendelea kule wamekuja sita wamebakiza watatu kwa sababu ili vikao viendelee kila nchi lazima kule iwe na *representation* ya *minimum* ya Wabunge watatu. Kwa hiyo wengine wote waliobaki wakiongozwa na Alhaji Kimbisa ni hawa hapa wamekuja kwa wapiga kura wao. (*Makofi*)

Mabalozi; Mwakilishi Mkazi wa *UNICEF* Shalini Bahuguna, karibu; Mwakilishi Mkazi wa *UNDP* Christina Musisi,

Mwakilishi Mkazi wa *UNHCR* Anthonio Jose, Balozi wa Pakistani Balozi Muhammad Saleem, Balozi wa Morocco Abdellah Benryane, Balozi wa Msumbiji- nchi jirani Monica Patricio, Balozi wa Ujerumani na Mwakilishi wa *EU* Regine Hess na Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa Zlatan Milišić. Ahsante sana. (*Makofi*)

Lakini pia ninao wageni wa Spika, Mke wa Askofu wa Dayosisi ya *Central Tanganyika* Mama Askofu Chilongani, amefuatana na Askofu mwenyewe wa Dayosisi ya *Central Tanganyika* Kanisa la Anglikana Dickson Chilongani, ahsante sana kufika Baba Askofu. (*Makofi*)

Katibu wa CCM wa Wilaya ya Kongwa Mbanga Michael, Katibu yuko wapi? Eee bwana ooh huyu mtu muhimu sana huyu. Naona Mheshimiwa Mnyika anamuangaliaa ndio huyo bwana. (*Makofi/Kicheko*)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa Dkt. Omary Nkulo, karibu sana; Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Mheshimiwa White Zuberi na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Kongwa Mwalimu Mussa Abdi, karibu sana Mwalimu Mussa Abdi. (*Makofi*)

Sasa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Ndugu Deo Ndejembie. Ahsante sana Mkuu wangu wa Wilaya kwa ushirikiano mkubwa ulionipa, nakushukuru sana. Na naona anaota ota kuja hapa. (*Makofi*)

Tunaye Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*) Florens Luoga, karibu na ahsante sana Gavana. *CAG* Ndugu Charles Kichere, ahsante sana *CAG* na kazi zake ni muhimu sana kwa kazi za Bunge. Pia yupo Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji Semistocles Kaijage. (*Makofi*)

Waheshimiwa makofi haya hayatoshi, mnaogopa uchaguzi, huyo ndio refa mkuu wa uchaguzi. (*Makofi*)

Naomba kumtambulisha kwenu Msajili wa Vyama vyatya Siasa Jaji Francis Mutungi, ahsante sana Mheshimiwa Jaji, sasa kazi yako ndio inaanza kabisaaa upya. (*Makofii*)

Sasa naomba niende upande wa vyombo vyatya ulinzi na usalama, nianze na Meja Jenerali Charles Mbuge - Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, ahsante Jenerali; Kaimu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevyia James Kaji; Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Brigedia Jenerali John Mbung'o naafikiri ni *Major General*sasa, mtanisamehe kama nimekosea. (*Makofii*)

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Ndugu John Masunga, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakala. (*Makofii/ Vigelegele*)

Kamishna Jenerali wa Magereza Meja Jenerali Suleiman Mzee; Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa Ndugu Diwani Athuman Msuya, ahsante sana Mkurugenzi kwa yote. Inspeksa Jenerali wa Polisi /GP Simon Sirro; Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Venance Mabeyo. (*Makofii*)

Tunaye pia Mkoo wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge na pia Katibu Mkoo Kiongozi Balozi John Kijazi. (*Makofii*)

Sasa nikaribie kwa viongozi wastaifu lakini nianze na wenza wa viongozi. Yupo Mama Spika, ahsante sana; yupo Mama Tunu Pinda ahsante sana; yupo Mama Regina Lowassa, ahsante sana; yupo Mama Asha Bilal, ahsante sana; yupo Mama Anna Mkapa, ahsante sana na yupo Mama Sitti Mwinyi, ahsante sana. (*Makofii*)

Viongozi wengine wastaifu tunaye Jaji Mkoo Mstaifu Jaji Mohamed Othman Chande, ahsante sana. Lakini tunaye Spika Mstaifu Mama Anna Makinda. (*Makofii*)

(Hapa Wabunge waliiimba mama mama huyo)

SPIKA: Wako Mawaziri Wakuu Wastaafu, Mheshimiwa Mizengo Pinda; yupo Waziri Mkuu Mstaafu Edward Lowassa; yupo Waziri Mkuu Mstaafu Frederick Sumaye na yupo Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Pia yupo Makamu wa Rais Mstaafu Dkt. Gharib Bilal. (*Makofi*)

Sasa nije kwa maraisi wastaafu, naanza na Rais Mstaafu Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, yupo Rais Mstaafu Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na yupo Rais Mstaafu Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Rais, pia ninao Wajumbe wa Sekretarieti ya CCM Taifa, kipekee ninao Wenyeviti wa Jumuiya, Mwenyekiti ya Vijana, Mwenyekiti wa Wazazi, Mwenyekiti wa UWT, ahsanteni sana Wenyeviti wetu. Lakini ninao Naibu Makatibu Wakuu wa CCM wote wawili Bara na Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Rais, pia tunaye Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma Ndugu Godwin Mkanwa, ahsante sana Mwenyekiti. (*Makofi*)

Sasa namalizia malizia tunaye Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa na pia mkiwa bado mmesimama tunaye Makamu wa Mwenyekiti CCM Bara, Ndugu Philip Mangula. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walimba CCM juu, CCM Juu)

SPIKA: Mheshimiwa Rais, ukishaona na Mzee Mangula amekuja ujuwe sasa kumekucha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Rais, kwa mara nyingine tunakushukuru sana kwa kuzungumza nasi na kupitia nasi umezungumza na Taifa, ni heshima kubwa sana umetupatia tunakushukuru kwa yote na mimi binafsi nakushukuru sana, sana, sana kwa jinsi

ambavyo kupitia kunisaidia umelisaidia sana Bunge hili. Basi mwisho sina cha kusema zaidi ya kusema *wabheja sana*. (*Makofi*)

Niwatakie kila kheri Waheshimiwa Wabunge wote, muende salama, Mwenyezi Mungu awatangulie, mfike salama, mkapange mipango yenu vizuri, basi Mwenyezi Mungu akijaalia mwezi Novemba hiyo tuje tuhesabiane hapa, turudishe *return* hapa, tuangalie vitu hivi, vitabakia hivi hivi au vitakuwa tofauti maana mengi yalise mwa kabla. (*Makofi*)

Basi kwa maneno hayo sasa naahirisha shughuli Bunge kama alivyosema Mheshimiwa Rais hadi wakati huo ambapo taratibu za Kikatiba zitakamilika kuitisha Bunge litakalofuata baada ya hapa ahsanteni sana kunisikiliza.

(Hapa Msafara wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoka Ukumbini ukiongozwa na Mheshimiwa Spika)

(Hapa Msafara wa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitoka Ukumbini ukiongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika)

(Hapa Msafara wa Majaji Wakuu wa Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitoka Ukumbini ukiongozwa na Wenye viti wa Bunge)

NDG. PATSON SOBHA: Waheshimiwa Wabunge, utaratibu ni kwamba tutaendelea kubaki ndani ya ukumbi wa Bunge mpaka mtakapotangaziwa utaratibu wa kutoka. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kubaki ndani ya ukumbi wa Bunge mpaka mtakapotangaziwa utaratibu wa kutoka.

(Saa 12:41 Mchana Bunge Lilahirishwa Rasmi Hadi hapo Litakapoitishwa Tena)